# Baadhi ya Hadithi za Mtume[saw]

Mfasiri

Jamil R. Rafiq

ISLAM
INTERNATIONAL
PUBLICATIONS LTD

# Baadhi ya Hadithi za Mtume[saw]

Selected Sayings of The Holy Prophet[saw] of Islam
(Swahili Translation)

**Mfasiri:**
Jamil R. Rafiq

Chapa ya Kwanza: 1988
Chapa ya pili: 2020

© Islam International Publications Ltd.

Kwa Maelezo Zaidi:

**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

**Kenya:**
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

Cover design: Salman Muhammad Sajid

ISBN: 978-1-84880-780-8
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

# YALIYOMO


Neno la Mbele ... i
Dibaji ... I
1. Nia na Matendo ... 1
2. Utukufu wa Mola Mtukuka ... 1
3. Umoja wa Pekee ... 2
4. Ukumbusho Bora: Kumkumbuka Mungu ... 2
5. Upendo wa Mola ... 5
6. Kurani Tukufu ... 7
7. Mfano Mwema wa Mtume[saw] wa Mungu ... 8
8. Nguzo za Islam ... 9
9. Sala Na Namna ya Kuabudu ... 10
10. Kufunga Saumu ... 13
11. Kuhiji ... 14
12. Zaka ... 15
13. Kuamrisha Mema na Kukataza Maovu ... 17
14. Kuwaita Watu kwa Allah ... 18
15. Maamrisho na Makatazo ... 19
16. Ndoa ... 20
17. Khulka Njema ... 21
18. Jamii ya Kiislamu ... 23
19. Kuwa Mwenye Shukurani kwa Watu ... 25
20. Kuwatendea Wema Wazazi ... 25
21. Ujirani ... 26
22. Kuwahurumia Wanyonge ... 26
23. Kusamehe ... 27
24. Adabu za Kula ... 27
25. Mavazi ... 28
26. Usafi ... 29
27. Husuda ... 29
28. Majivuno ... 30
29. Kuongopa ... 30
30. Kurudi Nyuma kwa Waislamu ... 31
31. Ujaji wa Imam Mahdi ... 32

# NENO LA MBELE

Hadhrat Khalifatul Masihi[rh] IV alifanya mpango wa kutoa kijitabu kuhusikana na baadhi ya Hadithi za Mtume Mtukufu[saw] kwa lugha mbali mbali, mojawapo ikiwa Kiswahili. Kwanza kabisa amri hii ilitekelezwa kwa Kiingereza, kisha tafsiri zake katika lugha kadhaa zilichapishwa.

Khalifa Mtukufu[rh] aliniagiza kutoa tafsiri yake kwa Kiswahili, nami nikaitika kwa haraka na mnamo mwaka 1988 tafsiri hii ilichapishwa kwa fadhili za Mwenyezi Mungu.

Wakati huu mkononi mwenu ni chapa yake ya pili ambayo herufi zake zilipangwa na Sheikh Ansar Hussain na pia katayarisha *fometi*. Twamshukuru kwa huduma hii alipotoa kwa kuchangamka.

Mola Mtukufu Awanufaishe wasomaji wa kitabu hiki.

Jamil R. Rafiq<br>
Wakilut Tasnif, Tahrike Jadid<br>
Rabwah, Pakistan — 7 Aprili 2020

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ [1]

# DIBAJI

Islam ni dini adhimu. Na siri ya adhama yake ni ukamilifu wa mafunzo ya Kurani Tukufu na kwamba Mwanzilishi wa Islam, Mtume Muhammad Mteule[saw], akatekeleza mafunzo hayo yote kikamilifu. Hivyo, yeye akawa mfano mtimilifu ulio hai wa yale aliyofundisha.

Uhusiano imara usioweza kuvunjika uliokuwa baina ya matendo yake na mafunzo yake ulitia alama isiyofutika katika Masahaba zake. Baada ya kufariki kwake, mkewe Bi Aisha[ra] alipoulizwa kuhusu maisha ya Seyidna Muhammad Mteule[saw], akajibu: *Kaana khulukuhul-Kur'an*, yaani khulka zake zilikuwa Kurani.

Kulikuwa hakuna upingamizi baina ya usemi wake na Neno la Mungu. Wahyi wake ulikuwa halisi bila ya kuwa na athari ya tamaa ya nafsi yake hata chembe. Kurani Tukufu inatoa ushuhuda kumhusu yeye hivi: "Wala hasemi kwa tamaa ya nafsi yake; siyo haya ila ni ufunuo uliofunuliwa." (53:4-5).

Si jambo la kushangaza, basi, kwamba Kurani Tukufu inamweka mbele ya watu kuwa mfano mkamilifu kwa wanadamu wote. Mwenyezi Mungu ndani ya Kurani

---

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na Mwingi wa Ukarimu.

Tukufu anasema: “Bila shaka mnao mfano mwema katika Mtume wa Mwenyezi Mungu”. (33:22)

Tumekwisha toa tayari kwa sura ya kitabu baadhi ya aya za Kurani Tukufu zinazoeleza mambo kadha ya muhimu kwa binadamu. Na sasa twaweka mbele ya wasomaji baadhi ya Hadithi za Mtume Muhammad[saw] kuhusu maisha, matendo na maneno yake. Kuzitalii Hadithi hizi kutaeleza kwa kifupi maisha ya Mtume[saw] ya kila siku, maombi yake, khulka zake na jinsi alivyohubiri.

Ijapokuwa baadhi ya Hadithi ziliwahi kuandikwa katika zama za uhai wake, lakini nyingi zaidi ziliandikwa takriban miaka 200 baada ya kufariki kwake. Ingawaje Hadithi nyingi zilikusanywa muda mrefu baada ya kufariki kwake, hata hivyo zaweza kutegemewa kabisa kwa sababu zifuatazo:

Kwa kuwa maneno ya Mtume Mtukufu[saw] yalikuwa yanaheshimiwa sana, hivyo yote aliyotamka yalikumbukwa kwa ghaibu pale pale na Masahaba zake na kukaririwa na kusimuliwa baina yao na kuzungumziwa mara nyingi mno.

Sababu ya pili ni kwamba kila alilotamka Mtume[saw] likachukuliwa kwa jazba ya kidini na upendo mkubwa. Kuligeuza kwa namna yoyote iwayo bali hata kutia tofauti sawa na chembe katika tamko lake kulihesabiwa kuwa dhambi itakayoulizwa na Mungu. Mwenyewe

alisema Mtume[saw], "Jahanamu ndiyo makao ya yule anayenasibisha kwangu nisiyoyanena."

Tatu, watu walipoeleza habari za kumhusu yeye ama kusimulia maneno yake kwa wengine, walikuwa na desturi kwamba mpokeaji wa ujumbe huo si tu alikumbuka kwa ghaibu yote aliyoambiwa bali pia akakumbuka jina la msimulizi pamwe na mambo kadha wa kadha kumhusu huyo mtu aliyesimulia Hadithi mbele yake, ili aweze kurejesha kwake kama simulizi lake likipingwa.

Jambo la nne lililo muhimu ni kwamba Waarabu walijulikana kuhusu kipawa chao kikubwa cha kukumbuka kwa ghaibu hata kabla hajaja Mtume[saw]. Halikuwa jambo la nadra kupatikana kati yao watu waliokumbuka kwa ghaibu beti 100,000 au zaidi za mashairi ya Kiarabu. Isitoshe, lilikuwa ni jambo la kawaida kukumbuka nasaba zao kikamilifu. Baada ya ujaji wa Mtume[saw], khulka za wafuasi wake zikawa za hali ya juu sana, na tabia ya kutia chumvi au kupiga chuku ikalaumiwa mno. Zaidi ya hayo, Kurani Tukufu si tu ilisisitiza kusema kweli bali na kuhakikisha pia usemi.

Matokeo ya hayo ni kwamba Hadithi za Mtume[saw] zilikusanywa kwa uangalifu wa hali ya juu mno usiofanyika katika utaratibu wa kukusanya matukio ya kihistoria.

Wakati wa kukusanya Hadithi hizi, wataalamu wa Kiislamu walikuwa waangalifu mno hata kuhusu mambo madogo madogo na walikuwa macho kuhusu usahihi wa kila jambo kiasi hiki kwamba mkusanyo wowote wa matukio ya Kihistoria hauwezi kabisa kulinganishwa na mkusanyo wa Hadithi za Mtume[saw] Kila msimulizi katika mfululizo wa wasimulizi wa kila hadithi ameainishwa katika vitabu vikubwa vya Hadithi. Bali na mtaala wa mienendo ya wasimulizi na uaminifu wao ukapanuka na ukawa uwanja maalum wa Elimu. Matokeo yake ni kwamba aina mpya ya utaalamu kuhusu mchanganuo wa Hadithi ukazalika mara ya kwanza katika historia ya binadamu.

Kwa manufaa ya wasomaji wale wanaojua kidogo kuhusu Islam yatubidi tueleze hapa kwamba miongoni mwa ma-ishirini ya vitabu vilivyoandikwa juu ya Hadithi, vitabu sita vyahesabiwa na wataalamu wa Kiislamu kuwa vya muhimu zaidi. Hivyo vyaitwa Sihaah Sittah, yaani vitabu sita vilivyo sahihi. Hadithi nyingi zaidi zilizoandikwa katika kijitabu hiki zinatokana na vitabu hivyo sita. Hapa chini twatoa maelezo kidogo kuhusu vitabu hivyo pamwe na waliovikusanya:

**SAHIHI BUKHARI:** Kitabu hiki kinahesabiwa kuwa sahihi zaidi baada ya Kurani Tukufu. Mwandishi wa kitabu hiki anaitwa Muhammad Ismail wa Bukhara, anayejulikana zaidi kwa jina Imam Bukhari. Alizaliwa

mwaka 194 Hijriyyah na kufariki mwaka 256 au sawa na kalenda ya Kikristo 816-878.

**SAHIH MUSLIM:** Kitabu cha pili katika umuhimu ni Sahih Muslim. Kiliandikwa na Muslim bin Al-Hajjaj mwenyeji wa Neshapur katika Khorasan. Alizaliwa mwaka 202 na kufariki 261 Hijriyyah.

**JAMI‘ TIRMIDHII:** Katika mpango huo, kitabu cha tatu ni Jami‘ Tirmidhii. Mwandishi wake ni Muhammad bin Isa alikuwa mwenyeji wa Tirmidh. Kazaliwa mwaka 209 na kufariki mwaka 279 Hijriyyah.

**SUNAN ABI DAWUD:** Cha nne ni Sunan Abi Dawud, kilichokusanywa na Sulaiman bin Ash‘ath ajulikanaye kwa jina Abu Dawud. (202-275 Hijriyyah).

**SUNAN IBN MAJAH:** Kinachohesabiwa cha tano kwa kutegemewa ni Sunan Ibn Majah. Kilikusanywa na Muhammad bin Yazid ibn Majah aliyezaliwa Quazwin, mji mashuhuri nchini Iran. (209-275 Hijriyyah).

**SUNAN NASAAI:** Kitabu cha sita ni Sunan Nasaai kilichokusanywa na Ahmad bin Shuaib anayejulikana kwa jina Nasaai kwani alitokana na mji wa Nasaa uliomo katika Khorasan.

**MUWATTA IMAM MALIK:** Zaidi ya Sihah Sita, kuna kitabu kingine tena cha umuhimu sana cha Hadithi za Mtume[saw] kinachoitwa Muwatta Imam Malik. Aliyekikusanya ni Malik bin Anas ajulikanaye kwa jina Imam Malik. Hiki hakipo miongoni mwa Shiha Sittah,

kwani kilihesabiwa ni kitabu hasa cha Fik-hi, maana Hadithi zilizokusanywa humo zaidi zinazungumzia masaala za kifik-hi. Usahihi wa Hadithi za kitabu hiki waweza kuzingatiwa kwa kuelewa kwamba Hadithi hizo zote zimepata kuandikwa katika Sahih Bukhari na Sahih Muslim. Daraja la Imam malik miongoni mwa wakusanyaji wa Hadithi ni la juu sana hata kwamba akapata lakabu ya Imamul-Muhaddithina, yaani Imam wa wakusanyaji wa Hadithi, na wakusanyaji wote wa Hadithi wanatambua daraja lake hili.

## 1. NIA NA MATENDO

Seyidna Umar[ra] anasimulia:

Nilimsikia Mtume Mtukufu[saw] akisema: “Matendo hutegemea nia pekee. Mtu atapata yale aliyonuia hasa. Kuhama kwa mtu anayenuia hasa kuhamia kwa Mungu na Mtume wake kutamwongoza kwa Mungu na Mtume wake. Lakini anayenuia vitu vya dunia ili kuvipata, au mwanamke ili kumwoa, basi kuhama kwake kutahesabiwa kwa kile alichokihamia.” (Bukhari).

Hadhrat Abdullah bin Umar[ra] anaeleza kwamba alimsikia Mtume Mtukufu[saw] akisema:

“Mwislamu wa kweli ni yule ambaye Waislamu wenginewanasalimika katika mikono yake na ulimi wake. Mhamiaji wa kweli ni yule anayeachana na yale yaliyokatazwa na Mungu.” (Bukhari).

## 2. UTUKUFU WA MOLA MTUKUKA

Hadhrat Abdullah bin Umar[ra] anasimuliwa kwamba Mtume Mtukufu[saw] alisema akitoa hotuba ya Ijumaa akiwa juu ya mimbari:

“Mbingu zimekunjwa katika mkono Wake wa kuume; Ameepukana na upungufu na Yu juu kabisa kuliko yale wamshirikishayo nayo.” Mtume Mtukufu[saw] akaongeza kueleza kwamba Mungu anasema, “Mimi Ndimi ninayo nguvu yote ya kurekebisha, Mtambuzi wa ukuu wangu, Mfalme, Niliye juu”. Mtume Mtukufu[saw] aliendelea kukariri maneno hayo kwa nguvu mpaka mimbari

ikaanza kutetemeka hata tukadhani itaanguka naye." (Musnad Ahmad).

Hadhrat Abu Huraira[ra] anasimulia kwamba Mtume Mtukufu[saw] alisema:

"Kuna mafungu mawili ya maneno yampendezayo mno Mwingi wa Rehema. Ni mepesi kutamka lakini mazito katika mizani, nayo ni: Ametukuka Mungu pamwe na sifa zake zote njema; Ametukuka Mungu Mwenye adhama." (Bukhari).

## 3. UMOJA WA PEKEE

Hadhrat Abu Huraira[ra] anasimulia kwamba Mtume Mtukufu[saw] alieleza ya kuwa Mwenyezi Mungu anasema:

"Mtumishi wangu ananikadhibisha ilhali haimpasi kufanya hivyo; ananitusi hali haimpasi kufanya hivyo. Kunikadhibisha kwake ni kusema: Akiisha niumba, Hatanifufua (baada ya mimi kufa). Na kunitusi kwake ni kudai kwamba Mungu Amepanga mwana, ilhali Mimi Sihitaji bali wote wanahitaji kwangu; Sikuzaa wala Sikuzaliwa, wala hakuna yeyote aliye sawa nami." (Musnad Ahmad).

## 4. UKUMBUSHO BORA: KUMKUMBUKA MUNGU

Hadhrat Jabir[ra] anasimulia kwamba alimsikia Mtume Mtukufu[saw] akisema:

"Njia bora zaidi ya kumkumbuka Mungu ni kutangaza: Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah. Na dua

bora zaidi ni kueneza: Sifa zote njema zinamhusu Allah". (Tirmidhi).

Hadhrat Abu Musa Al-Ash'ari[ra] anasimulia kwamba Mtume Mtukufu[saw] alisema:

"Mfano wa yule anayemkumbuka Mola wake na yule asiyemkumbuka Yeye ni mfano wa hai na maiti." (Bukhari).

Hadhrat Abu Musa[ra] anasimulia: Safari moja tulipokuwa tukisafiri pamoja na Mtume Mtukufu[saw], watu wakaanza kutamka kwa sauti ya juu "Allahu Akbar" (Mungu ni Mkuu). Hapo Mtume Mtukufu[saw] akasema:

"Enyi watu, ngojeni, shikeni njia ya kati. Kwani mnayemwita siyo kiziwi au asiyekuwapo; bali mwamwita Mwenye kusikia sana Aliye karibu, naye Yu pamoja nanyi." (Muslim)

Hadhrat Abu Huraira[ra] anasimulia ya kuwa Mtume Mtukufu[saw] alisema:

"Allah anao baadhi ya malaika wenye daraja kubwa ambao daima wanasafiri kuwatafuta watu wanaojumuika kwa kumkumbuka Allah. Wanapokwisha fikia hafla ambamo watu wanamkumbuka Mungu Mwenye Enzi, Malaika wanaungana nao kwa kutandaza mbawa zao juu yao, kila malaika akizunguka kwa kuruka juu ya mwenzake hadi nafasi iliyo baina ya ardhi na mbingu ya karibu inajaa na kuwepo kwao." (Hii ni mithali tu ya kueleza baraka za Mungu kuzidi kuongezeka kwa watu waanomkumbuka Mungu. Isichukuliwe kwa maana ya

dhahiri). Na watu wanapotawanyika, malaika nao hupanda juu mbinguni. Hao Mwenyezi Mungu Anawauliza, ilhali Anajua sana yaliyotendeka, “Mmetokea wapi”? Nao wanajib, “Tumefika kutoka kwa baadhi ya watumishi wako walioko ardhini waliokuwa wakikutukuza na kutangaza Ukuu wako na kutangaza Umoja wako na kutaja sifa zako na kukuomba.” Ndipo Mungu Anauliza, “Wakaniomba nini”? Malaika wanajibu, “ Wakaomba Pepo zake.” Mungu Anauliza, “Je, wameziona Pepo zangu”? Malaika wanajibu, “La, Mola wetu, hawajaziona Pepo zako”. Mungu Anasema, “Itakuwaje kama wakiisha ziona Pepo zangu!!” “Pia walitaka kujikinga Kwako”, Malaika wanaendelea. Mungu Anauliza, “Wanajikinga Kwangu katika nini”? “Katika Moto wako”, wanajibu. Allah Anauliza, “Je, wameuona Moto wangu?” Malaika wanajibu, “La, hasha”. “Ingekuwaje, kama wangeuona Moto wangu”, Asema Mungu. Hapo Malaika wanasema, “Walikuomba msamaha wako.” Mungu anajibu, “Nimekwishawasamehe mapema, bali nimekwishawapa yote waliyoniomba wakati wowote, na nimewakinga walivyonitaka”. Hapo Malaika wanasema, “Mola wetu, kati yao alikuwepo mmoja mwenye dhambi nyingi sana; yeye alikuwa akiwapitia tu na kuamua kukaa nao kidogo.” “Hata huyo Nimesamehe”, Asema Mungu, “hao ni watu waliobarakiwa hata kwamba anayewahi kukaa nao hawezi kubaki bila kupata baraka”. (Muslim).

# 5. UPENDO WA MOLA

Hadhrat Abu Dardaa[ra] anasimulia kwamba Mtume Mtukufu[saw] alisema kwamba Nabii Daudi[as] alikuwa akiomba ifuatavyo:

"E Mola, nijaalie mapenzi yako na mapenzi ya wale wanaokupenda, na mapenzi ya zile amali zitakazoniwezesha kupata mapenzi yako. E Mola wangu, Uyafanye mapenzi yako yawe yenye thamani zaidi kwangu kuliko uhai wangu na ahali zangu na hata kuliko maji baridi (kwa mtu aliyekurubia kufa kwa ajili ya kiu katika joto kali mno). (Tirmidhii).

Hadhrat Anas[ra] anasimulia ya kuwa Mtume Mtukufu[saw] alisema:

"Kuna mambo matatu ambayo yakipatikana kwa mtu, mtu huyo hupata utamu wa imani. Nayo ni kwamba Mwenyezi Mugnu na Mtume wake wawe wapenzi wake kuliko chochote kingine; kwamba ampende mwenzake kwa ajili ya Mungu tu pekee; kwamba baada ya Mungu kumwokoa katika ukafiri achukie kurejea katika kufuru jinsi anavyochukia kutupwa motoni". (Bukhari).

Hadhrat Abu Huraira[ra] anasimulia ya kwamba Mtume Mtukufu[saw] alisema:

"Kama mwaminio angetambua hasa wingi na ukali wa adhabu ya Mungu, angekata tamaa kabisa kupata Pepo. Na kama Kafiri angeelewa kikwelikweli wingi wa

rehema ya Mungu, asingekata tamaa kupata Pepo zake." (Muslim)

Hadhrat Waathila[ra] anasimulia ya kuwa Mtume Mtukufu[saw] alisema kwamba Mwenyezi Mungu anasema:

"Ninamtendea mtumishi Wangu jinsi anavyotazamia kwangu". (Bukhari).

Hadhrat Abu Huraira[ra] anasimuliwa kwamba Mtume Mtukufu[saw] alisema ya kuwa Mwenyezi Mungu anasmea:

"Namtendea mtumishi wangu jinsi anavyotazamia kwangu. Mwenyezi Mungu anafurahia toba ya mtumishi wake zaidi kuliko mmoja wenu kufurahia kupata ghafula ngamia wake aliyekuwa amepotea jangwani."

Mungu anasema, "Mtumishi wangu anaponisogelea sawa na shubiri moja, Mimi namsogelea sawa na dhiraa moja. Na akinisogelea sawa na dhiraa moja Miye namsogea sawa na dhiraa mbili. Na anaponijia akitembea, Mimi namkimbilia". (Muslim).

Hadhrat Abu Huraira[ra] anasimulia ya kwamba Mtume Mtukufu[saw] alieleza kuwa Mwenyezi Mungu anasema:

Kulikuwa na mtu mmoja aliyekuwa amejidhulumu sana (alitenda dhambi nyingi). Alipofikiwa na mauti akawausia wanawe akisema, "Nikiisha kufa nichomeni kisha nisageni na nitupeni katika upepo ndani ya bahari. Kwani, Wallahi naogopa kwamba Mungu akinishika ananiadhibu vikali asivyomwadibu yeyote awaye." Mtume[saw] akasema kwamba wale wanawe wakamtendea

hivyo. Lakini Mungu Akaiamuru ardhi, "Toa chembe zote ulizochukua za mwili wa mtu huyo." Basi mtu huyo akaletawa mbele ya Mungu, ndipo Mungu Akamwuliza, "Nini kilichokuhimiza kutenda hivyo?" Kasema, "Hofu yako au uchaji wako, E Mola wangu". Basi Mungu Akamsamehe. (Bukhari).

## 6. KURANI TUKUFU

Hadhrat Uthman bin 'Affan[ra] anasimulia kwamba Mtume Mtukufu[saw] alisema:

"Mbora wenu ni yule anayejifunza Kurani na kuwafundisha wengine." (Bukhari).

Hadhrat Ibn Abbas[ra] anasimulia kwamba Mtume Mtukufu[saw] alisema: "Mfano wa yule asiyekumbuka sehemu yoyote ya Kurani ni mfano wa nyumba iliyoachwa." (Trimidhii).

Hadhrat Zaid bin Arqam[ra] anasimulia:

"Siku moja Mtume Mtukufu[saw] aliinuka kutuhutubia; akamsifu Mungu na kumtukuza na kisha akatutolea mawaidha na kutusihi, kisha akasema:

'Ama badu, Enyi watu, mimi ni binadamu. Huenda nikafikiwa na mjumbe wa Mola wangu nami nikaitika. Ninawaachieni vitu viwili vya muhimu: Cha kwanza ni Kitabu cha Mungu ambamo mna mwongozo na nuru; basi shikamaneni na Kitabu cha Mungu. Kisha akasema, 'Na cha pili ni ahali zangu. Ninawatahadharisheni kuhusu ahali zangu, ninawatahadharisheni kuhusu ahali zangu, ninawataharisheni kuhusu ahali zangu.' (Muslim).

# 7. MFANO MWEMA WA MTUME[SAW] WA MUNGU

Hadhrat Abdullah bin Abi Aufa[ra] anasema:

"Mtume[saw] hakudharau au kubeua kutembea na mjane na maskini bali alikuwa akiwatimizia mahitaji yao." (Musnad Darmi).

Hadhrat Aisha[ra] anasimulia:

"Mtume Mtukufu[saw] hakumpiga yeyote abadan kwa mkono wake, si mwanamke wala si mtumishi, japo akapigana jihadi katika njia ya Mungu. Na hata akiudhiwa hakujilipiza kisasi. Lakini kilichoharamishwa na Mungu kikiondolewa heshima, hapo yeye akalipiza kisasi kwa ajili ya Mungu Mwenyezi. (Muslim).

Hadhrat Abu Said Khudri[ra] anasimulia:

"Mtume wa Mungu[saw] alikuwa akimlisha ngamia na kusimamia mambo ya nyumbani na kutengeneza viatu na kuzitilia viraka nguo, na kukamua maziwa ya kondoo na kula pamoja na mtumishi. Na mtumishi akichoka akisaga unga, yeye akamsaidia kusaga. Na hakuona haya kuchukua mwenyewe bidhaa za nyumbani kutoka sokoni kuzipeleka nyumbani. Alikuwa akipeana mikono na tajiri na maskini. Alikuwa akitangulia kutoa salam. Hakudharau kile alichoalikwa kwake hata kama ni tende mbovu. Alikuwa na tabia ya kula chakula cha kawaida, mwenye khulka njema, mkarimu wa tabia, mwenye kuishi vizuri na wengine, mchangamfu, mwenye

kutabasamu bila kucheka, si mwenye kukunja uso hata akihuzunika, mnyenyekevu lakini si dhalili, mkarimu si mbadhirifu, mwenye moyo mwepesi, mwenye huruma kwa kila Mwislamu. Alikuwa hateuki kwa shibe wala hakunyoosha mkono wake kwa tamaa." (Mishkaat).

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Musa Ash'ari[ra] kwamba safari moja Hadhrat Aisha[ra] alituonyesha vazi moja na shuka ya kiunoni ya kitambaa kinene na akasema, 'Mtume wa Mungu[saw] alipofariki alikuwa amevaa hizi.' (Bukhari).

## 8. NGUZO ZA ISLAM

Hadhrat Ibn Umar[ra] anasimulia ya kwamba Mtume Mtukufu[saw] alisema:

"Msingi wa Islam ni juu ya mambo matano:

Kushuhudia kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah na kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Allah.

Na kusimamaisha sala, (Ibada rasmi)

Na kuota zaka,

Kuhiji ka'ba,

Na kufunga saumu ya mwezi wa Ramadhani, (Bukhari).

Hadhrat Umar bin Khattab[ra] anasimuliwa:

"Tulikuwa tumekaa na Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] mara akatokea mtu mmoja mwenye nguo nyeupe sana na mwenye nywele nyeusi mno. Hakuonekana ni msafiri

wala yeyote kati yetu hakumjua. Akamjia Mtume[saw] na (kukaa karibu sana na Mtume[saw] hadi) goti lake likagusana na goti la Mtume[saw], kisha akasema, "Ewe Muhammad, imani ni nini?" Akasema Mtume[saw], "Imani ni kwamba umwamini Mwenyezi Mungu na malaika wake na vitabu vyake na mitume wake na siku ya mwisho na kadri njema na mbaya (kanuni kuhusu mema na mbabya)." (Tirmidhii).

## 9. SALA NA NAMNA YA KUABUDU

Imesimuliwa kumhusu Hadhrat Uthman bin 'Affan[ra] kwamba yeye aliagiza chombo cha maji (ili kutawadha). Basi akamimina maji juu ya viganja vyake vya mikono mara tatu na kuviosha. Kisha akaingiza mkono katika chombo na kuchota maji na kushukutua na kusafisha pua kisha kaosha uso mara tatu na mikono miwili mara tatu mpaka vikoni, kisha akapaka maji kichwani na ndipo akasafisha miguu yake hadi mafundoni mara tatu, kisha akasema, "Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] alisema, "atawadhaye nilivyotawadha na akasali rakaa mbili kwa makini kabisa husamehewa dhambi zake zilizotangulia." (Bukhari).

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira[ra] kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] alisema:

Je nisiwaambieni yale ambayo mkiyatenda Mwenyezi Mungu atawafutieni makosa yenu na kunyanyua madaraja. Masahaba wakasema, 'Naam, E Mjumbe wa

Mungu'. Kasema Mtume[saw] mambo yenyewe ndiyo haya:

"Kutawadha kikamilifu juu ya kutokupenda; na kutembea umbali mwingi kufika misikitini; na baada ya kusali tayari sala moja kuingojea sala nyingine. Na huku ndiko kufunga mafarasi mipakani, na huku ndiko kufunga mafarasi mipakani." (Muslim)

(Angalieni: Neno lililotumika katika Hadithi hii ni Ribaat ambalo tafsiri yake ni kufunga farasi mipakani ili kuilinda mipaka ya nchi; lakini kimfano ni kulinda hali njema ya kiroho. Katika Hadithi hii neno hili linahusiana na Ibada ya Kiislamu)

Hadhrat Aisha[ra] anasimulia akisema:

"Mtume[saw] wa Mwenyezi Mungu alikuwa akifungua sala kwa kutamka Takbira (kusema Allahu Akbar) na kisha akasoma Sura Al-Fatiha (Sura ya kwanza ya Kurani Tukufu). Na alipokuwa akiinama hakuinua sana kichwa chake wala hakukiinamisha kabisa, bali akakiweka katikati ya hali hizi mbili. Na alipoinua kichwa chake kutoka Rukuu, hakusujudu mpaka kwanza akasimama wima. Na alipoinua kichwa chake kutoka kwenye sujuda (ya kwanza) hakufanya sujuda (ya pili) mpaka kwanza akaketi sawasawa. Na baada ya kila rakaa mbili alikuwa akisoma *Attahiyyatu* (maneno maalum yanayojulikana) akikaa juu ya mguu wake wa kushoto uliotandazwa na akasimamisha mguu wake wa kuume. Na alikuwa akikataza kumfuata shetani, na pia kutandaza mikono

hadi viko viguse chini jinsi anavyotandaza mbwa mikono yake. Na alikuwa akimaliza sala kwa kusema 'Assalamu alaikum wa Rahmatullahi' (Amani na rehema za Mungu ziwe kwenu)." (Musnad Ahmad).

Imesimuliwa na Hadhrat Abdallah bin Mas'uud[ra] aliyesema: 'Nilimwuliza Mtume[saw] kitendo gani champendeza zaidi Mungu Mwenye Enzi? Kasema:

"Kusali katika wakati wake."

Nikasema: Tena kipi?

Kasema: Kuwatendea wema wazazi.

Nikasema: Tena kipi?

Kasema: Kufanya jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu. (Bukhari)

Hadhrat Amr bin Shuaib anasimulia kutoka kwa baba yake ambaye anasimulia kutoka kwa babu yake ya kwamba Mtume Mtukufu[saw] alisema:

"Waamuruni watoto wenu kusali wanapokuwa wenye umri wa miaka saba; na wanapokuwa wenye umri wa miaka kumi mwapige wasiposali na kuwatenganisha walale katika vitanda mbali mbali." (Abu Dawud)

Anasimulia Hadhrat Fatima Az-Zahraa[ra] kwamba Mtume Mtukufu[saw] alipokuwa akiingia msikitini alikuwa anaomba kwa kusema:

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu. Na amani iwe kwa Mtume wa Mungu. E Mola wangu, nighofirie dhambi zangu na nifungulie milango ya rehema zako.”

Na alipokuwa akitoka kutoka msikitini aliomba hivi:

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu. Amani iwe kwa Mtume wa Mungu. E Mola wangu, nighofirie dhambi zangu na nifungulie milango ya fadhili zako.” (Musnad Ahmad)

## 10. KUFUNGA SAUMU

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira[ra] kwamba Mtume Mtukufu[saw] alisema:

“Mungu Mwenye Enzi na Utukufu anasema kwamba vitendo vyote vya binadamu ni kwa ajili yake, isipokuwa saumu. Saumu hufungwa kwa ajili yangu pekee, Nami Ndimi malipo yake. Saumu ni ngao (ya kujikinga na maovu). Basi mmoja wenu akifunga siku fulani, yeye asizungumze yasiyo na maana wala asipige kelele. Na kama mtu anamtukana au kupigana naye, basi yeye (mfunga saumu) aseme tu: Nimefunga saumu.” (Bukhari)

Hadhrat Abu Huraira[ra] anasimulia ya kuwa Mtume Mtukufu[saw] alisema:

“Asiyeachana na kuongopa na kudanganya, Mungu hana haja ya kwamba yeye mtu huyo aache chakula chake na kunywa kwake.” (Bukhari)

Imesimuliwa na Hadhrat Aisha[ra] ya kwamba Mtume Mtukufu[saw] alikuwa anashinda msikitini (kukaa itikafu) katika kumi la mwisho la Ramadhani mpaka Mwenyezi Mungu Akamfisha, kisha wakeze wakaendelea kukaa itikafu baada yake. (Bukhari)

## 11. KUHIJI

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira[ra] aliyesema kwamba Mtume Mtukufu[saw] alituhutubia na akasema:

"Enyi watu, Mwenyezi Mungu Amefaradhisha juu yenu kuhiji, basi hijini." Hapo mtu mmoja akauliza, "Je, kila mwaka?" Mtume[saw] akakaa kimya mpaka mtu huyu akarudia swali lake mara tatu. Ndipo Mtume[saw] akasema, "Kama ningesema Naam, ingewajibika wala msingeiweza." Akaendela kusema, "Msiulize nisiyowaelezeni. Kwani waliangamia wale wa kabla yenu kwa sababu ya kuuliza kwao sana lakini kuwaasi Manabii wao. Basi ninapowaamuruni jambo fulani, litekelezeni sawa na uwezo wenu wote; na nikiwakatazeni kitu fulani, mjitenge nacho." (Muslim)

Anasimulia Hadhrat Abu Huraira[ra] ya kuwa Mtume Mtukufu[saw] alisema:

"Anayehiji kwa ajili ya Mungu na hatumii midomo michafu wala haasi, atarejea ilhali hana dhambi jinsi alivyokuwa siku mama yake alipomzaa." (Mishkaat)

## 12. ZAKA

Hadhrat Mu'adh[ra] anasimulia akisema:

"Mtume wa Mungu[saw] alinituma (akinifanya hakimu wa sehemu fulani) na akaniambia:

"Utakutana na baadhi ya watu miongoni mwa Ahli Kitab. Basi uwaite kwa kushuhudia kwamba hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah na kwamba mimi ni Mtume wa Allah. Wakikubali, hapo uwaelimishe kwamba Mwenyezi Mungu Amefaradhisha juu yao sala tano kila siku, usiku na mchana. Wakikubali hiyo pia, uwafundishe kwamba Mwenyezi Mungu Amewawekea faradhi ya kutoa sadaka inayochukuliwa kutoka kwa matajiri na kuwarudishia maskini kati yao. Wakikubali hiyo, jiepushe na kuchukua mali zao zilizo bora zaidi. Na iogope dua ya aliyedhulumiwa, kwani hakuna kinga baina yake na baina ya Allah." (Bukhari)

Anasimulia Hadhrat Khuraim bin Fatik[ra] kwamba Mtume[saw] alisema:

"Anayetoa chochote katika njia ya Mwenyezi Mungu, huandikiwa malipo mara mia saba." (Tirmidhii)

Hadhrat Anas[ra] anasimulia kwamba Hadhrat Abu Talha[ra] alikuwa tajiri zaidi kati ya Ma-ansar wa Madina (yaani watu wa Madina waliosilimu kabla Mtume[saw] kuhamia huko). Utajiri huo ulitokana na bustani za mitendo ambazo kati ya hizo bustani aliyoipenda zaidi ilikuwa ile ya Biruhaa iliyotazamana na msikiti. Mtume

wa Mungu[saw] alikuwa akiingia humo na kunywa maji yake mazuri. Anas anasema, "Iliposhuka aya hii: Hamwezi kupata wema hasa mpaka mtoe katika yale mnayoyapenda, Talha[ra] akaja kwa Mtume wa Mungu[saw] na akasema, "E Mjumbe wa Mungu, hakika Mwenyezi Mungu Amekuteremshia aya isemayo: 'Hamwezi kupata wema hasa mpaka mtoe katika yale mnayoyapenda; na mali ninayopenda zaidi ni bustani ile ya Biruhaa; basi hiyo natoa kama sadaka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, nikitarajia Mungu atakipokea kitendo changu hiki chema na kukiweka kwa akhera. E Mjumbe wa Mungu, itumie jinsi Atakavyokuongoza Mungu." Akasema Mtume wa Mungu[saw]: 'Vizuri sana! Hii ni mali yenye manufaa, hii ni mali yenye manufaa. Nami nimesikiliza uliyosema. Lakini naona uwatolee hiyo jamaa zako wa karibu.' Abu Talha[ra] akasema, "Nitafanya E Mjumbe wa Mungu, ulivyosema." Basi akaigawa baina ya jamaa zake wa karibu na binamu zake." (Bukhari)

Hadhrat 'Adii bin Hatim[ra] anasimulia kwamba Mtume wa Mungu[saw] alisema:

"Jikingeni na moto walau kwa kutoa nusu ya tende." (Bukhari)

Anasimulia Hadhrat Aisha[ra] kwamba Mtume wa Mungu[saw] alisema:

"Mkarimu yuko karibu na Mungu, karibu na watu, karibu na Pepo, mbali na Mtoto. Na bahili yuko mbali na Mwenyezi Mungu, mbali na watu, mbali na Pepo,

karibu na Moto. Mjinga mkarimu ni mpendwa zaidi wa Mungu kulio mwenye ibada aliye bahili." (Qushairiyyah)

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira[ra] akisema aliyesema kwamba mtu mmoja alimwuliza Mtume Mtukufu[saw] akisema:

"E Mjumbe wa Mungu, sadaka gani ni kubwa kimalipo?" Kasema, "kwamba utoe sadaka ilhali u mzima, mwenyewe unahitaji hiyo mali, ukiogopa umaskini na kutamani kutajirika. Wala usingoje hadi roho ifikapo kooni ndipo ukasema fulani apewe kiasi kadha na fulani apewe kiasi kadha, kwani hiyo (mali yako) imekwisha kuwa ya fulani (kwa sababu unakufa sasa na wengine watairithi). (Mishkaat)

## 13. KUAMRISHA MEMA NA KUKATAZA MAOVU

Hadhrat Hudhaifa[ra] anasimulia kwamba Mtume[saw] alisema:

"Naapa kwa Yule ambaye uhai wangu umo mkononi mwake kwamba hamna budi ninyi kuamrisha mema na kukataza maovu ama huenda Mungu akawaleteeni adhabu kutoka Kwake. Hapo mtamwomba dua lakini haitapokelewa kwenu." (Tirmidhii)

lmesimuliwa na Nu'man bin Bashir[ra] kwamba Mtume[saw] alisema:

"Mfano wa yule anayezingatia mipaka ya Mwenyezi Mungu na yule anayeivuja hiyo mipaka ni kama mfano

wa wale waliopiga kura ili kupata nafasi katika safina. Baadhi yao wakapata nafasi katika sitaha ya juu na wengine katika sitaha ya chini. Na wale walio kwenye sitaha ya chini wakitaka maji walitakiwa kuwapitia walio kwenye sitaha ya juu. Ndipo wakasema kama tungetoboa katika sehemu yetu tusingewaudhi walio juu yetu. Sasa walio kwenye sitaha ya juu wakiwaacha kutenda walivyotaka wale wa chini wataangamia wote; na kama wakiwazuia watasalimika, bali watasalimika wote." (Bukhari)

## 14. KUWAITA WATU KWA ALLAH

Hadhrat Sahl bin Sa'd[ra] anasimulia ya kuwa Mtume Mtukufu[saw] alimwambia Hadhrat Ali[ra]:

"Wallahi, kama Mungu akimwongoza mtu mmoja pekee kwa njia yako, hiyo ni bora kwako kuliko ngamia wekundu (ambao wana thamani kubwa)." (Muslim)

Hadhrat Abu Huraira[ra] anasimulia kwamba Mtume wa Mungu[saw] alisema:

"Mtu ambaye anawaelekeza watu kwenye ukweli, atapata thawabu sawa na thawabu ya wale wote watakaokubali ukweli kwa sababu ya kuelekezwa kwake bila kuwapunguzia malipo yao. Kadhalika yule mtu ambaye anawashawishi wengine kutenda dhambi atabeba dhambi za wale wote watakaofanya dhambi kwa sababu ya kushawishiwa naye, bila ya

kuwapunguzia adhabu wale waliotenda dhambi." (Muslim)

Hadhrat Anas[ra] anasimulia ya kuwa Mtume wa Mungu[saw] alisema:

"Ifanyeni dini iwe rahisi kuifuata; wala msiifanye kuwa ngumu. Kadhalika, elezeni dini kwa njia ya kupendeza, wala msiifanye watu waichukie." (Muslim)

## 15. MAAMRISHO NA MAKATAZO

Hadhrat Abu Tha'laba[ra] Al-Khushanii Jurthuum bin Naashir anasimulia kwamba Mtume wa Mungu[saw] alisema:

"Mwenyezi Mungu Amefaradhisha mambo kadha, msiyapuuze. Ameweka mipaka fulani, msiiruke. Amekataza mambo kadha msiyasogee. Amenyamaa kuhusu mengine kadha kwa sababu ya kuwahurumieni si kwa kuyasahau; hivyo, msiulize-ulize kuhusu hayo bila sababu." (Dar Qutni)

Hadhrat N'uman bin Bashir[ra] anasimulia kwamba yeye alimsikia Mtume wa Mungu[saw] akisema:

"Yaliyo halali yamebainishwa na pia yaliyo haramu yamewekwa wazi. Baina ya hayo mawili kuna mengine yasiyofafanuliwa, wasiyajue wengi hayo yako upande gani. Anayejiweka mbali nayo huilinda imani yake na hesima yake. Aingiaye katika yale yalio ya shaka, huenda akaingia katika yaliyokatazawa. Yeye mtu huyo ni kama mchungaji anayewaacha kuondoo zake wajilishe kando

ya eneo lililokatazwa, ilhali yaelekea sana kondoo hao waliingilie eneo hilo. Kumbukeni, kila mfalme analo eneo lililokatazwa lisiingiliwe. Na eneo lililokatazwa kuingiliwa la Mungu ni mambo Aliyoharamisha. Sikilizeni, kuna sehemu maalum katika mwili ambayo ikiwa na afya, mwili mzima huwa na afya. Na hiyo inapougua, mara mwili mzima huugua. Kumbukeni, sehemu hiyo ni moyo." (Muslim)

## 16. NDOA

Hadhrat Abu Huraira[ra] anasimulia kwamba Mtume wa Mungu[saw] alisema:

"Mtu humwoa mwanamke kwa sababu ya mambo manne: Utajiri wake, nasaba yake, uzuri wa sura yake na ucha-Mungu wake. Utangulizi ucha-Mungu wake; uwe mnyenyekevu." (Bukhari).

Hadhrat Abu Huraira[ra] anasimulia kwamba Mtume wa Mungu[saw] alisema:

"Karamu mbovu zaidi ya arusi (walima) ndiyo ile ambamo matajiri pekee wanaalikwa na wenye hali ndogo hawaalikwi. Yule anayealikwa (na mtu mwenye hali ndogo) na akakataa (kwa sababu ya kiburi), anamwasi Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake." (Muslim)

Hadhrat Ibn Umar[ra] anasimulia ya kuwa Mtume wa Mungu[saw] alisema:

"Kinachomchukiza zaidi Mungu Mwenye Enzi kati ya vile vilivyo halali ni talaka." (Abu Dawud).

Hadhrat Aisha[ra] anasimulia ya kuwa Mtume wa Mungu[saw] alisema:

"Mbora wenu ni yule aliye mbora kwa ahali zake. Nami ni mbora wa wale wote kati yenu wanaowatendea wema ahali zao." (Abu Dawud).

## 17. KHULKA NJEMA

Hadhrat Jabir[ra] anasimulia ya kwamba Mtume Mtukufu[saw] alisema: "Hakika wapendwa wangu zaidi miongoni mwenu na watakaonikurubia kimakao siku ya Kiyama ni wale wenye khulka njema. Na wenye kunichukiza zaidi kati yenu na watakaokuwa mbali nami siku ya Kiyama ni wale wenye kupayuka na wenye kuwadhihaki wengine na wale 'mutafaihikuun'. Masahaba wakasema, E Mjume wa Mwenyezi Mungu, twaelewa wapayukao na wafanyao dhihaka, lakini 'Mutafaihiquun' ni akina nani? Kasema Mtume[saw] hao ndio wenye kiburi." (Tirmidhii).

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira[ra] ya kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] alisema:

"Nimetumwa ili kutimiliza khulka zilizo bora." (As-Sunanul-Kubra).

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira[ra] ya kwamba Nabii[saw] alisema:

"Yule amwondoleaye mumini shida katika shida za kidunia, Mwenyezi Mungu atamwondolea shida katika shida za siku ya Kiyama. Na atakayemfariji mwenye dhiki, Mungu Atampa faraja duniani na akhera. Na amsitiriye Mwislamu udhaifu wake, Mungu Atamsitiri katika dunia na akhera. Na Mwenyezi Mungu humsaidia mtu, maadamu huyo mtu anamsaidia nduguye. Na anayekanyaga njia ili kujitafutia elimu humo, Mwenyezi Mungu Atamrahisishia njia ya kwenda Peponi. Na watu hawajumuiki katika nyumba mojawapo ya Mungu wakisoma Kitabu cha Mungu na kufundishana hicho wao kwa wao isipokuwa utulivu huwashukia, rehema huwafunika, Malaika huwazunguka, na Mwenyezi Mungu Huwataja kwa wale walio karibu naye. Na yule ambaye vitendo vyake vimemchelewesh, nasaba yake haitamharakisha kwenda mbele." (Muslim).

lmesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira[ra] ya kuwa Mjumbe wa Mungu[saw] alisema:

Hakika Mwenyezi Mungu Atasema siku ya Kiyama, 'Ee mwana wa Adamu, niliugua lakini hukuniangalia'. Yeye atajibu, 'Ee Mola wangu, ningekuangalije ilhali U Mola wa walimwengu'. Mungu atasema, 'Je, hujui kwamba mtumishi wangu fulani aliugua lakini hukumwangalia. Hujui kwamba kama ungeenda kumwangalia ungenikuta kule kwake. Ee mwana wa Adamu, nilikuomba chakula lakini hukunilisha'. Yeye atasema, 'Ee Mola wangu, ningekulishaje ilhali U Mola wa walimwengu?' Mungu

Atasema, 'Je, hukujua kwamba mtumishi wangu fulani alikuomba chakula lakini hukumlisha. Je, hujui kama ungemlisha ungemkuta karibu nami? Ee mwana wa Adamu, nilikuomba maji lakini hukuninywesha'. Yeye atasema, 'Ee Mola wangu, ningekunyweshaje ilhali U Mola wa walimwengu!' Mungu Atasema, 'Mtumishi wangu fulani alikuomba maji lakini hukumnywesha. Kama ungemnywesha maji ungemkuta karibu nami'. (Muslim)

Alisema Nabi[saw]:

"Hakika hamwezi kuwatajirisha watu kwa mali zenu; basi, wafarijini kwa ucheshi wa uso na khulka njema." (Risalah Qushairiyyah)

## 18. JAMII YA KIISLAMU

Hadhrat Anas[ra] anasimulia ya kwamba Nabii Mtukufu[saw] alisema:

"Yeyote miongoni mwenu hawezi kuwa mumini sawasawa mpaka ayapende kwa nduguye yale anayopenda kwa nafsi yake mwenyewe." (Bukhari).

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira[ra] aliyesema kwamba Mtume Mtukufu[saw] alisema:

"Ewe Hadhrat Abu Huraira[ra], uwe mcha-Mungu, utakuwa mwenye ibada zaidi kuliko watu wote. Na uridhike na hali yako, utakuwa mwenye shukurani kuliko watu wote. Na upende kwa watu yale

unayopenda kwa nafsi yako, utakuwa muumini. Na umtendee jirani yako vizuri sana, utakuwa Mwislamu. Na usicheke sana, kwani kucheka kwa wingi huua roho.” (lbn Majah)

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Yusuf Abdullah[ra] bin Salaam anayesema kwamba nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] akisema: “Enyi watu, enezeni desturi ya kuamkiana kwa ‘Assalamu alaikum,’ na walisheni (wenye njaa), na watendeeni wema jamaa wa karibu, na salini ilhali watu wamelala, mtaingia Peponi kwa amani.” (Tirmidhii)

lmesimuliwa na Hadhrat Ibn Mas‘uud[ra] kwamba Mtume wa Mungu[saw] alisema:

“Mnapokuwa watatu, basi wawili wasizungumze kwa kumwacha yule wa tatu mpaka mchanganyikane na watu wengine, kwani jambo hili litamhuzunisha.”' (Muslim).

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira[ra] kwamba:

“Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] alipokuwa akipiga chafya, alikuwa akiweka mkono wake ama kitambaa chake juu ya kinywa chake na kwa njia hii akapunguza nguvu ya chafya”. (Tirmidhii).

## 19. KUWA MWENYE SHUKURANI KWA WATU

lmesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira^ra ya kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu^saw alisema:

"Asiyewashukuru watu hamshukuru Mungu." (Tirmidhii)

## 20. KUWATENDEA WEMA WAZAZI

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira^ra:

Mtu mmoja alimjia Mtume^saw wa Mwenyezi Mungu^saw na akasema, Ee Mjumbe wa Mungu, ni nani mwenye haki zaidi kati ya watu wote ambaye napaswa kukaa naye vizuri zaidi?' Kasema, 'Mamako'. Kasema, 'Nani tena?' Kajibu, 'Mamako'. Akasema, 'Kisha nani?' Kajibu, 'Mamako'. Huyo akauliza, 'Tena nani?' Akajibu, 'Babako'.

Katika riwaya nyingine imesimuliwa hivi: "Ewe Mjumbe wa Mungu, nani ana haki zaidi kwamba nikae naye vizuri? Akasema: Mamako, mamako, mamako, kisha babako, kisha jamaa anayekukurubia zaidi na kadhalika." (Bukhari).

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira^ra kwamba Mtume^saw alisema:

"Ni mwenye bahati mbaya, ni mwenye bahati mbaya, ni mwenye bahati mbaya yule aliyewapata wazazi wake, wote wawilli au mmojawapo, katika uzee, lakini hakupata kuingia Peponi." (Muslim).

## 21. UJIRANI

Imesimuliwa na Hadhrat Ibn Umar[ra] na Hadhrat Aisha[ra] kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] alisema:

Malaika Jibrili alidumu kunisihi kumhusu jirani mpaka nikadhani atamfanya kuwa mrithi." (Bukhari).

lmesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira[ra] kwamba Mtume Mtukufu[saw] alisema:

"Anayemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, asimwudhi jirani yake. Na anayemwamini Mungu na siku ya mwisho, amheshimu mgeni wake. Na anayemwamini Mungu na siku ya mwisho, aseme la kheri ama anyamaze kimya." (Bukhari).

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira[ra] kwamba Mtume[saw] alisema:

"Wallahi hajaamini, Wallahi hajaamini, Wallahi hajaamini." Akaulizwa, 'Nani?' Kasema, "Yule ambaye jirani yake hayuko salama kutokana na shari yake." (Bukhari).

## 22. KUWAHURUMIA WANYONGE

lmesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira[ra] kwamba Mtume Mtukufu[saw] alisema:

"Kuna watu wengine wenye nywele za matimutimu zenye vumbi wanaofukuzwa milangoni, lakini (ni wacha-Mungu kiasi hiki kwamba) kama wakiapa kwa Mungu, Mungu huwatimizia kiapo chao." (Muslim).

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Dardaa[ra] aliyesema kwamba yeye alimsikia Mtume wa Mungu[saw] akisema:

"Nitafuteni baina ya wale walio wanyonge kati yenu, kwani mnaruzukiwa na kusaidiwa kwa hao wanyonge miongoni mwenu." (Tirmidhii).

## 23. KUSAMEHE

Imesimuliwa na Hadhrat Mu'adh bin Anas[ra] kutoka kwa Mtume wa Mungu[saw] kwamba yeye alisema:

"Khulka bora zaidi ni kwamba uimarishe uhusiano na yule anayeuvunjilia mbali, na umpe akunyimaye, na umsamehe akutukanaye." (Musnad Ahmad).

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira[ra] kwamba Mtume wa Mungu[saw] alisema:

"Sadaka haipunguzi mali; wala mtu hasamehi adhulumiwapo ila Mwenyezi Mungu humzidishia heshima." (Musnad Ahmad).

## 24. ADABU ZA KULA

Imesimuliwa na Hadhrat Aisha[ra] kwamba Mtume wa Mungu[saw] alisema:

"Mmoja wenu anapoanza kula, inampasa ataje jina la Mungu Mtukufu (aseme Bismillahi). Na kama alisahau kutaja jina la Mungu Mtukufu mwanzoni mwa kula, basi (akumbukapo) aseme: Bismillahi Awwalahu wa

Akhirahu (yaani, kwa jina la Mungu mwanzoni mwake na mwishoni mwake).” (Tirmidhii).

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Said[ra] aliyesema kwamba Nabii[saw] alipokuwa akila na akinywa alikuwa anaseme:

“Sifa zote njema zamhusu Mungu Aliyetulisha na kutunywesha na kutujaalia kuwa Waislamu.” (Tirmidhii).

## 25. MAVAZI

lmesimuliwa na Hadhrat Hudhaifa[ra] akisema:

Mtume[saw] alitukataza tusivae nguo za hariri wala za zari; wala tusinywe katika vyombo vya fedha na dhahabu, na akasema, “Hivyo ni kwao (makafiri) katika dunia, navyo vitakuwa kwenu huko akhera.” (Muslim).

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Said Khudri[ra] aliyesema kwamba Mtume wa Mungu[saw] alipokuwa akivaa nguo mpya alikuwa akiitaja jina, kama vile ‘kilemba’, ‘shati’ au ‘joho’, na kisha akaomba hivi:

“Ee Mota wangu, sifa zote njema ni zako. Wewe umenivisha hii. Nami nakuomba unijalie kheri yake na kunijalia kupata ile shabaha bora ambayo kwayo hii imetengenezwa. Na ninajikinga kwako katika shari yake na shabaha ile mbaya ambayo kwayo hii imetengenezwa.” (Tirmidhii).

## 26. USAFI

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Musa Ash'ari[ra] kwamba Mtume wa Mungu[saw] alisema:

"Usafi ni sehemu ya imani." (Muslim).

lmesimuliwa na Hadhrat Aisha[ra] kwamba Mtume[saw] alisema:

"Kupiga mswaki ni njia ya kusafisha kinywa na kupata radhi ya Mola". (Nasaai).

## 27. HUSUDA

Imesimuliwa na Hadhrat Ibn Umar[ra] kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] alisema:

"Msihusudiane wala msizidishane bei kwa kudanganya wala msibughudhiane wala msitengane, wala mmoja wenu asipige bei ya kitu ilhali mwingine anapatana na mwenzake bei ya kitu hicho; na kuweni, enyi watumishi wa Mungu, ndugu nyinyi kwa nyinyi. Mwislamu ni ndugu wa Mwislamu, hamdhulumu wala hamdunishi wala hamwachi bila kusaidia. Ucha-Mungu ndio hapa" — na akaashiria kwenye kifua chake na kasema hayo mara tatu — (na akaendelea kusema) "'inamtosha mtu kuwa na shari kwamba amdhalilishe nduguye Mwislamu. Ni haramu kwa kila Mwislamu damu na mali na heshima ya Mwislamu mwingine." (Muslim).

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira[ra] kwamba Mtume[saw] alisema:

"Jiepusheni na husuda, kwani husuda inakula mema kama moto unavyokula kuni au akasema majani." (Abu Dawuud).

## 28. MAJIVUNO

Imesimuliwa na Hadhrat Abdullah bin Mas'uud[ra] kwamba Mtume[saw] alisema:

"Hataingia Peponi yule aliye na majivuno moyoni mwake hata sawa na chembe." Mtu mmoja akasema, "Hakika mtu anapenda kwamba nguo zake ziwe nzuri na viatu vyake viwe vizuri!" Kajibu, "Hakika Mwenyezi Mungu ni Mzuri na anapenda uzuri. Lakini majivuno ndiyo kukataa ukweli kwa kiburi na kuwahakirisha watu." (Muslim).

## 29. KUONGOPA

lmesimuliwa na Hadhrat Abdullah[ra] ya kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] alisema:

"Shikamaneni na kusema kweli, kwani ukweli huongoza kwenye wema na wema huongoza kwenye Pepo. Na mtu anadamu kusema kweli na kuiriaria hata anaandikwa kuwa Siddik (mkweli sana) mbele ya Mungu.

Na jiepusheni na uwongo, kwani uwongo huongoza kwenye maovu, na maovu huongoza kwenye moto. Na mtu hudumu kusema uwongo na kuuriaria mpaka anaandikwa mbele ya Mungu kuwa Kadh-dhab (mwongo sana)." (Muslim).

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Bakrah[ra] kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] alisema:

"Je, nisiwaambieni dhambi zilizo kubwa?" Tukasema, "Naam, Ee Mjumbe wa Mwenyezi Mungu." Akasema, "Kumshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote, kuwaasi wazazi." Na Mtume[saw] aliyekuwa ameegemea akakaa sawasawa na kasema, "Sikilizeni, na kuongopa." Na aliendelea kukariri hayo mpaka tukasema laiti angenyamaza. (Bukhari).

## 30. KURUDI NYUMA KWA WAISLAMU

lmesimuliwa na Abdullah bin Amr[ra] kwamba Mtume wa Mungu[saw] alisema:

"Yataujia Umati wangu mambo sawasawa kabisa na yale yaliyowajia wana wa Israeli jinsi kiatu kimoja kinavyofanana na kiatu kingine, kiasi hiki kwamba hata kama alikuwapo kati yao mmojawapo aliyemzini mamake mzazi hadharani, basi na kati ya Umati wangu pia atapatikana atakayetenda hivyo. Na hakika wana wa Israeli waligawanyika katika makundi 72, lakini Umati wangu utafarakana kuwa madhehebu 73, lakini yote hayo yataingia motoni isipokuwa kundi moja tu." Masahaba wakasema, "Ni lipi hilo, Ee Mjumbe wa Mwenyezi Munga." Kajibu, "Lile litakalofuata sunna yangu na ya masahaba zangu. (Tirmidhii).

Imesimuliwa na Hadhrat Ali[ra] kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] alisema:

"Ni karibu ziwafikie watu zile zama ambapo halitabaki katika Islam isipokuwa jina, wala halitabaki katika Kurani ila maandiko; misikiti yao itaendewa na watu wengi lakini kimwongozo itakuwa mitupu. Masheikh wao watakuwa viumbe wabaya zaidi chini ya mbingu; fitina zitatoka kutoka kwao na zitawarejea." (Mishkaat).

## 31. UJAJI WA IMAM MAHDI

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira[ra], akisema: "Tulikuwa tumekaa na Mtume[saw] iliposhuka Sura Al-Jumu'ah. Na aliposoma sehemu hii ya aya: *Wa Akhariina Minhum Lamma Yalhakuu Bihim* (yaani 'Na kwa wengine wao walio bado kuungana nao'), mtu mmoja akauliza, "Nani hao, Ee Mjume wa Mungu (ambao wametajwa hapa kwamba wataungana na Masahaba zako baadaye)?" (Kidhahiri katika aya hii habari ya ujaji wa Mtume[saw] mara ya pili katika zama zingine umetabiriwa). Mtume[saw] hakujibu, mpaka huyo mtu akauliza mara mbili au mara tatu. Na kati yetu alikuwepo Salmaan[ra] Mwajemi pia. Mtume[saw] akaweka mkono wake juu ya Salmaan[ra] na akasema: "Kama imani ingekuwa kule kwenye kilimia, mtu au watu wangeipata wanaotokana na hao." (Muslim, Bukhari).

lmesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira[ra] kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] alisema:

"Naapa kwa Yule ambaye uhai wangu umo mkononi mwake kwamba karibuni atatokea kati yenu mwana wa Mariamu akiwa Mwamuzi mwadilifu na atavunja

msalaba na kuua nguruwe, na ataondoa vita (vya dini sawa na mwongozo wa Mungu) na atagawa mali mpaka mtu yeyote hataipokea. Katika zama hizo sujuda moja pekee itakuwa bora kuliko dunia na yilivyomo humu." Kisha Hadhrat Abu Huraira[ra] akasema (Haya ni maoni ya Hadhrat Abu Huraira[ra] siyo rnaneno ya Mtume[saw]): Someni mkipenda aya hii: Na hakuna yeyote katika watu wa Kitabu ila ataliamini kabla ya kifo chake, naye (Masihi) siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao (4:160). (Bukhari).

"Sikilizeni, hatakuwa Nabii wala Mtume baina yangu mimi na baina na Isa bin Mariamu, naye atakuwa Khalifa wangu katika Umati wangu baada yangu. Sikilizeni, yeye ataua Dajjal, atavunja msalaba, ataondoa jizya, kwani havitakuva vita (vya dini). Sikilizeni, yeyote atakayempata amfikishie salamu (zangu). (Tabarani).

lmesimuliwa na Hadhrat Anas[ra] kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] alisema:

"Yeyote miongoni mwenu atakayeonana na lsa bin Mariamu, basi amfikishie salamu zangu." (Durri Manthuur).

lmesimuliwa na Hadhrat Thauban[ra] kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] alisema:

"Mkimpata (Mahdi) mfanye baiati yake (mwungane naye) hata mkitakiwa kutambaa juu ya theluji kwa

kumfikia, kwani yu Khalifa wa Mungu na Mahdi." (Ibn Majah, Kitabul Fitan).

lmesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira[ra] kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] alisema:

"Mtakuwaje atakaposhuka kati yenu Ibn Mariamu ilhali yu lmam wenu kutoka miongoni mwenu." Katika riwaya nyingine akasema, 'naye atawaongozeni kutoka miongoni mwenu'. (Bukhari).

lmesimuliwa na Hadhrat Muhammad bin Ali[ra] kwamba:

"Hakika kwa ajili ya Mahdi wetu kuna alama mbili ambazo hazijatokea (kwa kuhakikisha ukweli wa Mdai yeyote) tangu ziumbwe mbingu na ardhi. Nazo ni hizi: Mwezi utapatwa tarehe ya kwanza (kati ya tarehe za kupatwa mwezi) katika Ramadhan, na jua litapatwa tarehe ya kati (miongoni mwa tarehe zake za kupatwa) mnamo mwezi huo huo wa Ramadhan. Na alama hizi hazijatokea (kuhakikisha ukweli wa Mdai) tangu kuumbwa mbingu na ardhi." (Sunan Dar Qutni).

(Maelezo: Mwezi hupatwa tarehe 13, 14 na 15 za tarehe za kimwezi. Katika hizo siku, tarehe ya kwanza ya kupatwa mwezi ni tarehe 13. Kadhalika jua hupatwa tarehe mojawapo kati ya 27, 28 na 29 za kimwezi. Tarehe ya kati katika hizo ni tarehe 28. Kwa hivyo, Hadithi ya Mtume[saw] inamaanisha kupatwa mwezi tarehe 13 na jua tarehe 28 katika Ramadhan kama alama ya kudhihirika kwa Imam Mahdi.)

lmesimuliwa na Hadhrat Sulaiman bin Amr bin Al-Ahwas[ra] akisema baba yangu aliyehudhuria Hija ya mwisho pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] alinihadithia kwamba:

Mtume[saw] alimsifu Mwenyezi Mungu na kumtukuza Yeye na akasihi na kutolea mawaidha kisha akasema: "Siku gani ni tukufu zaidi, siku gani ni tukufu zaidi, siku gani ni tukufu zaidi?" Masahaba wakasema, "Siku ya Hija kubwa, Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu." Hapo akasema, "Basi, damu zenu, mali zenu na heshima zenu zina utukufu sawa na utukufu wa siku yenu hii katika mji wenu huu ndani ya mwezi wenu huu. Sikilizeni, hakuna yeyote atakayeulizwa isipokuwa kwa dhambi zake yeye mwenyewe; wala baba hataulizwa kuhusu dhambi za mwanaye, wala mwana kwa dhambi za babake. Sikilizeni, Mwislamu ni ndugu wa Mwislamu; hivyo, si halali kwa Mwislamu kujichukulia mali ya nduguye isipokuwa ile aliyomhalalishia mwenyewe. Sikilizeni, pesa zote za riba za siku za ujinga zafutiliwa mbali; raslimali ni zenu tu, msidhulumu wala msidhulumiwe. Naam, riba ya Abbas bin Abdil Muttalib (jamaa wa karibu wa Mtume[saw]) pia imefutiliwa yote moja kwa moja. Sikilizeni, kila damu iliyomwagwa kabla ya Islam imefutiliwa mbali isilipizwe kisasi. Na damu ya kwanza ninayofuta iliyomwagwa katika siku za ujinga ni damu ya (Rabi'a bin) Harith bin Abdil Muttalib (Jamaa wa karibu wa Mtume[saw]) aliyekuwa ananyonyeshwa katika kabila la Bani Laith na akauawa na Hudhail.

Sikilizeni, mwapaswa kuusiana kuwatendea wanawake wema, kwani hao ni amana kwenu (nanyi mtaulizwa juu yao); hamna madaraka juu yao isipokuwa kiasi hiki tu kwamba wao ni amana tu kwenu Naam, wakitenda mabaya dhahiri waacheni peke yao vitandani na kuwapiga lakini si vikali. Na wakiwatiini, msiwatafutie njia ili muwe wakali kwao. Sikilizeni, ninyi mnazo haki kadha juu ya wake zenu; na wake zenu nao wanazo haki kadha juu yenu. Na haki yenu juu ya wake zenu ni kwamba waishi maisha mema na wasiwaruhusu nyumbani mwenu wale msiowataka waingie. Sikilizeni, na haki zao juu yenu ni kwamba mwafanyie hisani kuwavisha na kuwalisha. (Tirmidhii).